



Zana Rahisi Ya Kadi Ya Alama Za Umaskini Uganda

Mark Schreiner

10 Agosti 2021

This document and a [data-collection tool](#) are in English at scorocs.com
Ekiwandiiko kino [ekirimu ebikunganyiziddwa](#) aba scorocs.com kiri mu Luganda
Waraka huu na [zana ya kukusanya data](#) ziko kwa lugha ya Kiswahili kwenye scorocs.com

Zana rahisi ya kutathmini umaskini ya Kadi ya Alama za Umaskini ya Scorocs® (*Scorocs® Simple Poverty Scorecard®-brand poverty-assessment tool*) ni mbinu nafuu, na wazi ya kutumiwa na miradi ya kuwasaidia maskini nchini Uganda ili kuthibitisha na kuboresha utendakazi wao wa kijamii ili kupata kujua washiriki wao vyema zaidi. Majibu ya maswali 10 vya kadi ya alama yanaweza kukusanya kwa takribani dakika 10 na kisha kutumika kukadiria viwango vya umaskini vya mshiriki kulingana na matumizi, kufuatilia mabadiliko katika viwango vya umaskini, au kuwapanga washiriki kwa makundi kwa ajili ya shughuli tofauti.

Dokezo la toleo

Kadi hii mpya ya alama ya Uganda inategemea data za mwaka wa 2016/17. Inachukua nafasi ya kadi za zamani za alama zilizo kwenye Schreiner (2011a na 2015a) ambazo zinategemea data za mwaka wa 2009/10 na za 2012/13. Kwa sababu viwango vya umaskini nchini Uganda zilizongezeka kutoka mwaka wa 2012/13 hadi 2016/17, na kwa sababu kadi za alama hazirekodi vyema maongezeko ya umaskini, watumiaji watatahadharishwa kutokadiria mabadiliko katika viwango vya umaskini vya muda kwa kutumia maelezo msingi kutoka kwenye kadi ya zamani ya alama na ufuatiliaji kutoka kwenye kadi mpya ya alama.

Shukrani

Data zimetolewa kwenye shirika la Uganda's Bureau of Statistics. Shukrani kwa Yanni Chen, James Muwonge, na Vincent Fred Ssennono. Imetafsiriwa na [SwahiliSpace](#).

Scorocs® Simple Poverty Scorecard® Tool

Nambari ya mahojiano: _____ **Jina** _____ **Kitambulishi** _____
 Tarehe ya mahojiano: _____ Mshiriki: _____
 Nchi: **UGA** Ajenti wa nyanjani: _____
 Kadi ya alama: **003** Kituo cha huduma: _____
 Sampuli ya uzito: _____ Idadi ya jamaa wa kaya: _____

Swali

| Swali | Jibu | Alama |
|---|---|------------------------------------|
| 1. Kaya iko katika eneo lipi? | A. Busoga, Bukedi, au Karamoja B. Central I, Central II, Elgon, au West Nile C. Acholi, Bunyoro, Kampala, Kigezi, au Teso D. Tooro E. Ankole, au Lango | 0 5 9 12 16 |
| 2. Kuna jamaa wangapi katika kaya? | A. Saba au zaidi B. Sita C. Tano D. Nne E. Tatu F. Wawili G. Mmoja | 0 2 4 8 12 20 30 |
| 3. Kiongozi mwanamke (au mke mkubwa zaidi wa kiongozi mwanamume) anaweza kusoma na kuandika kwa ufasaha kwa lugha yoyote? | A. Hakuna kiongozi mwanamke (wala mke wa kiongozi mwanamume) B. La C. Ndiyo | 0 3 5 |
| 4. Kuna jamaa ye yote wa kaya anayeenda shule ya kibinafsi au shule ambayo inaendeshwa na shirika la kidini, NGO, au shirika lingine lolote lisilo la serikali? | A. La B. Ndiyo | 0 7 |
| 5. Katika miezi 12 iliyopita, kuna jamaa wa kaya aliye pata mapato kutokana na ukulima wa mimea au ufugaji mifugo? | A. Uku lima wa mimea, lakini si ufugaji mifugo B. Hakuna uku lima wa mimea wala ufugaji mifugo C. Ufugaji Mifugo (bila kujali uku lima wa mimea) | 0 4 5 |
| 6. Aina ya nyenzo msingi iliyotumika sana katika ujenzi wa sakafu? (<i>kama ulivyoona</i>) | A. Matope, matope maalum, mbao, au nyingine B. Sementi na mchanga, zege, matofali, mawe ya matofali, au mawe | 0 9 |
| 7. Kaya inatumia aina ipi ya choo sana sana? | A. Hakuna choo/kichaka/mifuko ya plastiki/ndoo/n.k., choo cha shimo (bila kifuniko na bila silabu), au nyingine B. Choo cha shimo (chenye kifuniko na/au silabu), Ecosan (choo cha mbolea), choo cha VIP, au choo cha maji | 0 4 |
| 8. Kwa sasa jamaa wa kaya wana simu ngapi za mkononi ambazo zinafanya kazi? | A. Hakuna B. Mmoja C. Wawili au zaidi | 0 5 11 |
| 9. Kila jamaa wa kaya ana angalau kiatu kimoja ambacho ni kizuri kuvaliwa? | A. La B. Ndiyo | 0 6 |
| 10. Katika siku saba zilizopita jamaa wa kaya walipata wastani wa milo mingapi kwa siku? | A. Mbili au chache B. Tatu au zaidi | 0 7 |

Karatasi ya Kazi ya Ukurasa wa Nyuma: Jamaa wa Kaya

Jaza kichwa cha kadi ya alama kwanza. Jumuisha kitambulishi cha kipekee cha mahojiano (ikiwa kinajulikana), tarehe ya mahojiano, na sampuli ya uzito wa mshiriki (ikiwa unajulikana). Kisha rekodi jina kamili na nambari ya utambulisho ya kipekee ya mshiriki huyo (ambaye huenda akawa ni tofauti na anayejibu), ya ajenti wa nyanjani wa mshiriki (ambaye huenda akawa tofauti na mhoji), na ya kituo cha huduma ambacho mshiriki hutumia (ikiwa kipo na ikiwa kinajulikana). Weka mduara kwenye jibu la swali la kwanza la kadi ya alama kulingana na eneo ambapo kaya inaishi. “Mwongozo wa Mahojiano” unaorodhesha wilaya kulingana na eneo.

Kisha umsomee mhojiwa: Tafadhali niambie majina ya kwanza (au majina ya utani) ya jamaa wote wa kaya yako, ukianzia na kiongozi na mwanandoa wake (mkubwa zaidi) (ikiwa yupo). Kaya *ni mtu mmoja au kundi la watu—bila kujali uhusiano wa damu au ndoa—ambao kwa angalau miezi sita ya miezi 12 kabla ya mahojiano waliishi pamoja katika makazi moja na wamekula pamoja, ambao wanatambua mwanamume au mwanamke mmoja kuwa kiongozi wa kaya hiyo, na ambao wanachukuliwa kuwa kitu kimoja.*

Andika jina la kwanza au jina la utani la kila jamaa, ukianzia na kiongozi na mwanandoa (mkubwa zaidi) wa kiongozi (ikiwa yupo). Onyesha kiongozi na mwanandoa wake (ikiwa yupo) ni yupi. Rekodi idadi ya jamaa wa kaya kwenye kichwa cha kadi ya alama karibu na “Idadi ya jamaa wa kaya:”. Kisha uweke mduara kwenye jibu la swali la kwanza la kadi ya alama linalohusu idadi ya jamaa wa kaya.

Soma maswali yanayofuata kwa sauti (isipokuwa swali la sita linalohusu aina ya sakafu), na uweke alama kwenye majibu ya mhojiwa. Kila wakati ukumbuke na ufuate maagizo yaliyo kwenye “Mwongozo wa Mahojiano”.

| Jina la kwanza au jina la utani? | Kiongozi au mwanandoa wa kiongozi? |
|---|--|
| 1. | Kiongozi (mwanamume) Kiongozi (mwanamke) |
| 2. | Mke mkubwa zaidi wa kiongozi mwanamume Mume wa kiongozi mwanamke Mwingine |
| 3. | Mwingine |
| 4. | Mwingine |
| 5. | Mwingine |
| 6. | Mwingine |
| 7. | Mwingine |
| 8. | Mwingine |
| 9. | Mwingine |
| 10. | Mwingine |
| 11. | Mwingine |
| 12. | Mwingine |
| 13. | Mwingine |
| Idadi ya jamaa: | — |

Mwongozo wa Mahojiano

Marejeleo yaliyonukuliwa hapa yametlewa kwenye:

Uganda Bureau of Statistics. (2016) “Interviewers Manual of Instructions for the UNHS 2016/17” [Mwongozo].

Maagizo msingi ya mahojiano

Kadi ya alama inaweza kujaza kwenye karatasi nyanjani, na majibu kujazwa baadaye kwenye kwenye kompyuta au katika hifadhidata yako binafsi. Vinginevyo, zana ya kukusanya data ya Scorocs iliyo kwenye wingu inafanya kazi vyema katika kivinjari mtandao au kama programu ya simu ya Android, ambayo inawezesha uingizaji data nyanjani au ofisini. Ikiwa hakuna intaneti, basi data inahifadhiwa kwenye kifaa mpaka wakati kutakuwa na intaneti. [Pakua](#) zana ya kukusanya data, au [uliza kuhusu akaunti ya kibinafsi](#).

Kadi ya alama inapaswa kuwasilishwa na mhoji aliyeptia mafunzo ya kufuata Mwongozo huu.

Kwanza jaza kichwa cha kadi ya alama na “Karatasi ya Kazi ya Ukurasa wa Nyuma”, ukifuata maelekezo yaliyo kwenye “Karatasi ya Kazi ya Ukurasa wa Nyuma”.

Katika kichwa cha kadi ya alama, jaza idadi ya jamaa wa kaya kulingana na orodha ambayo wewe na mhoji mlitengeneza kama sehemu ya “Karatasi ya Kazi ya Ukurasa wa Nyuma”.

Usiulize swali la kwanza la kadi ya alama wazi wazi (“Kaya iko katika eneo lipi?”). Badala yake, jaza jibu kulingana na maarifa yako kuhusu eneo ambapo kaya inaishi. Hapa chini, Mwongozo huu unaorodhesha wilaya 112 katika mwaka 2016/17 na maeneo yake husika.

Kwa njia sawia, usiulize swali la pili la kadi ya alama wazi wazi (“Kuna jamaa wangapi katika kaya?”). Badala yake, weka alama kwenye jibu kulingana na idadi ya jamaa wa kaya ambao uliorodhesha kwenye “Karatasi ya Kazi ya Ukurasa wa Nyuma”.

Muulize mhojiwa maswali yote yaliyosalia moja kwa moja, isipokuwa swali la sita (“Aina ya nyenzo msingi iliyotumika sana katika ujenzi wa sakafu?”). Kwa swali hili moja, wewe kama mhoji unapaswa ujaribu kutazama na urekodi nyenzo kuu ya ujenzi wa sakafu bila kumuuliza mhojiwa swali hili moja kwa moja. Ikiwa hauna uhakika kabisa kuhusu jibu, basi muulize mhojiwa swali hili.

Mwongozo jumla wa kufanya mahojiano

Pitia mwongozo huu kwa uangalifu, na uubebe unapofanya kazi. Fuata maagizo yaliyo katika mwongozo huu (pamoja na agizo hili).

Kumbuka kwamba mhojiwa katika mahojiano haya si lazima awe jamaa wa kaya ambaye anashiriki katika mpango wako.

Vivyo hivyo, ajenti wa nyanjani arekodiwe katika kichwa cha kadi ya alama si lazima awe mhoji kama wewe ambaye anaendesha mahojiano. Badala yake, ajenti wa nyanjani ni mwajiriwa wa mpango wa kuwasaidia maskini ambao mshiriki ana uhusiano nao ambao unaendelea. Ikiwa hakuna ajenti kama huyo, basi acha nafasi hizo zikiwa tupu kwenye kichwa cha kadi ya alama.

Soma kila swali bila kuruka neno lolote, kwa mpangilio uliowekwa kwenye kadi ya alama (isipokuwa swali la sita, “Aina ya nyenzo msingi iliyotumika sana katika ujenzi wa sakafu?”).

Unapoweka alama kwenye jibu la swali la kadi ya alama, andika alama kwenye safu ya “Alama” na kisha uweke mduara kwenye jibu la maneno, alama iliyochapwa, na alama za kuandikwa kwa mkono, kama hivi:

| | | |
|---|--|------------|
| 3. Kiongozi mwanamke (au mke mkubwa zaidi wa kiongozi mwanamume) anaweza kusoma na kuandika kwa ufasaha kwa lugha yoyote? | A. Hakuna kiongozi mwanamke (wala mke wa kiongozi mwanamume) | 0 |
| | B. La | 3 3 |
| | C. Ndiyo | 5 |

Ili kusaidia kupunguza hitilafu, unapaswa:

- Kuandika alama zinazolingana na jibu katika safu ya mwisho upande wa kulia
- Weka mduara kwenye jibu lililochapwa, alama zilizochapwa, na alama za kuandikwa kwa mkono

Wakati suala linapoibuka ambalo halijaangaziwa katika Mwongozo huu, suluhu yake inapaswa kutolewa na mhoji na mhojiwa, kwani hiyo ndio kawaida ya UBOS ya Uganda katika UNHS ya mwaka 2016/17. Yaani, mpango unaotumia kadi hii ya alama haupaswi kutoa ufanuzi au sheria zozote (isipokuwa zile zilizo katika Mwongozo huu) za kutumiwa na wahoji wake wote. Chochote ambacho hakijaangaziwa moja kwa moja katika Mwongozo huu kiachiwe uamuzi wa kila mhoji na mhojiwa binafsi.

Usimsomee mhojiwa machaguo ya majibu. Badala yake, soma swalii, na uachie hapo; subiri jibu. Mhojiwa akiomba ufanuzi au akisitasita au aonekanae kuchanganyikiwa, soma swalii hilo tena na utoe usaidizi kulingana na Mwongozo huu au jinsi wewe kama mhoji unavyoona inafaa.

Kwa ujumla, unapaswa kukubali majibu yanayotolewa na mhojiwa. Hata hivyo, mhojiwa akisema kitu chochote—au ukiona au ukihisi jambo—ambacho kinaashiria kwamba jibu hilo si sahihi, kwa mhojiwa hana uhakika, au kwamba mhojiwa angependa kuopata usaidizi ili kubaini jinsi atajibu, Basi unapaswa kusoma swalii tena na kumpa usaidizi unaoona ni mwafaka kulingana na Mwongozo huu.

Ilhali majibu mengi kwa maswali yaliyo katika kadi ya alama yanaweza kuthibitishwa, mara nyingi hauhitaji kuthibitisha majibu. Unapaswa kuthibitisha tu ikiwa kuna jambo linaashiria kwamba huenda jibu likawa si sahihi na hivyo basi uthibitishaji huenda ukaimarisha ubora wa data. Kwa mfano, unaweza kuchagua kuthibitisha endapo mhojiwa atasitasita, anaonekana kuwa na uwoga, au vinginevyo anaashiria kwamba anadanganya, amechanganyikiwa, au hana uhakika. Vivyo hivyo, uthibitishaji huenda ukawa mwafaka ikiwa mtoto katika kaya inayohojiwa au jirani aseme kitu ambacho hakilingani na jibu la mhojiwa. Pia uthibitishaji ni mzuri ukiona kitu ambacho kinaashiria kwamba jibu si sahihi, kama vile kitu ambacho mhojiwa anasema hamili, au mtoto anayekula chumbani ilhali hakuhesabiwa kama jamaa wa kaya hiyo.

Kwa ujumla, matumizi ya kadi ya alama yanapaswa kufanana kwa karibu zaidi kadri iwezekanavyo na matumizi ya UNHS ya mwaka 2016/17 na UBOS ya Uganda. Kwa mfano, mahojiano yanapaswa kufanywa ana kwa ana na mhoji aliyeptitwa mafunzo katika makazi ya mshiriki kwa sababu UBOS ilifanya jambo sawia katika UNHS ya mwaka 2016/17.

Tafsiri:

Kufikia wakati wa uandishi huu, kadi yenye ya alama, “Karatasi ya Kazi ya Ukuura wa Nyuma”, na Mwongozo huu zinapatikana tu kwa lugha za Kiingereza, Kiluganda, na Kiswahili. Bado hakuna tafsiri rasmi na za kitaalamu za lugha nyingine kuu zinazozungumzwa nchini Uganda. Watumiaji wanapaswa kutazama scorocs.com ili kuona ni tafisri zipi zimefanywa tangu undishi huu kufanywa.

Ikiwa hakuna tafsiri rasmi na ya kitaalamu ya lugha inayotakikana, basi watumiaji wanapaswa kuwasiliana na Scorocs ili kupata usaidizi wa kutengeneza tafsiri hiyo.

Mhojiwa anapaswa kuwa nani?

Kumbuka kwamba mhojiwa si lazima awe jamaa wa kaya ambaye anashiriki katika mpango wako (ingawa mhojiwa pia anaweza kuwa jamaa huyo).

Kulingana na ukurasa wa 4 wa *Mwongozo*, “Jamaa yejote wa kaya ambaye ni mtu mzima mwenye uwezo anaweza kuwa mhojiwa katika mahojiano ya kaya.”

Kulingana na ukurasa wa 11 wa *Mwongozo*, “Mhojiwa anapaswa kuwa kiongozi wa kaya. Ni lazima uulize maswali machache ili kumtambvua kiongozi wa kaya. Ikiwa kiongozi wa kaya hayupo, basi mtu mwengine anayetenda kama kiongozi wa kaya anapaswa kuhojiwa. Mhojiwa huyu anapaswa kuwa jamaa wa kaya ambaye ni mtu mzima na anapaswa kuwa na uwezo wa kutoa maelezo hitajika kuhusu jamaa wengine wa kaya. Kumbuka kwamba jamaa wengine wanaweza kusaidia kwa kuongezea maelezo katika maswali yanayowahusu.”

Kiongozi wa kaya ni nani?

Kumbuka kwamba kiongozi wa kaya anaweza au akakosa kuwa jamaa wa kaya ambaye anashiriki katika mpango wako (ingawa kiongozi pia anaweza kuwa jamaa huyo).

Kulingana na ukurasa wa 12 wa *Mwongozo*, “*kiongozi wa kaya ni mtu anayechukuliwa na jamaa wa kaya kama kiongozi wao*. Mara nydingi, kiongozi wa kaya ni yule anayedhibiti mapato na gharama za kaya na ambaye ana maarifa zaidi kuhusu jamaa wengine wa kaya. Yeye atatajwa unapouliza swali ‘Kiongozi wa kaya hii ni nani?’ Unapaswa kukubali uamuzi wa jamaa wa kaya wanapomtambua kiongozi wao.

“Ni lazima kuwe na kiongozi mmoja pekee wa kaya. Endapo zaidi ya mtu katika kaya anadai kuwa kiongozi, au endapo jamaa wa kaya wanatoa kauli zinazokinzana kuhusu kiongozi wa kaya ni nani, basi kuna uwezekano mkubwa kwamba pale kuna kaya mbili au zaidi, badala ya moja. Katika tukio kama hilo, tumia vigezo vilivyotolewa vyatubaini ni nani jamaa wa kaya unayohoji.”

Miongozo ya kila swali katika kadi ya alama

1. Kaya iko katika eneo lipi?

- A. Busoga, Bukedi, au Karamoja
- B. Central I, Central II, Elgon, au West Nile
- C. Acholi, Bunyoro, Kampala, Kigezi, au Teso
- D. Tooro
- E. Ankole, au Lango

Isipokuwa iwe inabidi, usimuulize mhojiwa swali hili wazi wazi. Badala yake, jaza jibu kulingana na maarifa yako kuhusu wilaya (na pia eneo) ambapo kaya inaishi.

Kila moja ya wilaya 112 ambazo Uganda ilikuwa nazo katika mwaka 2016/17 inalingana na eneo fulani (ukurasa wa 90, UBOS, 2018). Jedwali lililo hapa chini lina orodha ya wilaya zilizoainishwa kulingana na alfabeti na maeneo yake husiani.

| Wilaya | Eneo |
|---------------|-------------|
| Abim | Karamoja |
| Adjumani | West Nile |
| Agago | Acholi |
| Alebtong | Lango |
| Amolatar | Lango |
| Amudat | Karamoja |
| Amuria | Teso |
| Amuru | Acholi |
| Apac | Lango |
| Arua | West Nile |
| Budaka | Bukedi |
| Bududa | Elgon |
| Bugiri | Busoga |
| Buhweju | Ankole |
| Buikwe | Central II |
| Bukedea | Teso |
| Bukomansimbi | Central I |
| Bukwo | Elgon |
| Bulambuli | Elgon |
| Buliisa | Bunyoro |
| Bundibugyo | Tooro |

| Wilaya | Eneo |
|---------------|-------------|
| Bushenyi | Ankole |
| Busia | Bukedi |
| Butaleja | Bukedi |
| Butambala | Central I |
| Buvuma | Central II |
| Buyende | Busoga |
| Dokolo | Lango |
| Gomba | Central I |
| Gulu | Acholi |
| Hoima | Bunyoro |
| Ibanda | Ankole |
| Iganga | Busoga |
| Isingiro | Ankole |
| Jinja | Busoga |
| Kaabong | Karamoja |
| Kabale | Kigezi |
| Kabarole | Tooro |
| Kaberamaido | Teso |
| Kalangala | Central I |
| Kaliro | Busoga |
| Kalungu | Central I |
| Kampala | Kampala |
| Kamuli | Busoga |
| Kamwenge | Tooro |
| Kanungu | Kigezi |
| Kapchorwa | Elgon |
| Kasese | Tooro |
| Katakwi | Teso |
| Kayunga | Central II |
| Kibaale | Bunyoro |
| Kiboga | Central II |
| Kibuku | Bukedi |
| Kiruhura | Ankole |
| Kiryandongo | Bunyoro |
| Kisoro | Kigezi |
| Kitgum | Acholi |
| Koboko | West Nile |

| Wilaya | Eneo |
|---------------|-------------|
| Kole | Lango |
| Kotido | Karamoja |
| Kumi | Teso |
| Kween | Elgon |
| Kyankwanzi | Central II |
| Kyegegwa | Tooro |
| Kyenjojo | Tooro |
| Lamwo | Acholi |
| Lira | Lango |
| Luuka | Busoga |
| Luwero | Central II |
| Lwengo | Central I |
| Lyantonde | Central I |
| Manafwa | Elgon |
| Maracha | West Nile |
| Masaka | Central I |
| Masindi | Bunyoro |
| Mayuge | Busoga |
| Mbale | Elgon |
| Mbarara | Ankole |
| Mitooma | Ankole |
| Mityana | Central II |
| Moroto | Karamoja |
| Moyo | West Nile |
| Mpigi | Central I |
| Mubende | Central II |
| Mukono | Central II |
| Nakapiripirit | Karamoja |
| Nakaseke | Central II |
| Nakasongola | Central II |
| Namayingo | Busoga |
| Namutumba | Busoga |
| Napak | Karamoja |
| Nebbi | West Nile |
| Ngora | Teso |
| Ntoroko | Tooro |
| Ntungamo | Ankole |

| Wilaya | Eneo |
|---------------|-------------|
| Nwoya | Acholi |
| Otuke | Lango |
| Oyam | Lango |
| Pader | Acholi |
| Pallisa | Bukedi |
| Rakai | Central I |
| Rubirizi | Ankole |
| Rukungiri | Kigezi |
| Sembabule | Central I |
| Serere | Teso |
| Sheema | Ankole |
| Sironko | Elgon |
| Soroti | Teso |
| Tororo | Bukedi |
| Wakiso | Central I |
| Yumbe | West Nile |
| Zombo | West Nile |

2. Kuna jamaa wangapi katika kaya?

- A. Saba au zaidi
- B. Sita
- C. Tano
- D. Nne
- E. Tatu
- F. Wawili
- G. Mmoja

Usimuulize mhojiwa swali hili wazi wazi. Badala yake, weka alama kwenye jibu kulingana na idadi ya jamaa wa kaya ambao uliorodhesha kwenye “Karatasi ya Kazi ya Ukurasa wa Nyuma”.

Kulingana na ukurasa wa 11–14 wa *Mwongozo*, “*kaya inabainishwa kama mtu au kundi la watu ambao wamekuwa wakiishi na kula milo yao pamoja kwa angalau miezi sita ya miezi 12 kabla ya mahojiano haya.*

“Kwa hivyo, jamaa wa kaya anabainishwa kulingana na makazi yake ya kawaida. Kuna matukio sharti hili halitumiki kama ilivyoelezewa hapa chini:

- Kategoria zifuatazo za watu wanazingatiwa kama jamaa wa kaya hata ingawa wameishi [na kula milo] na kaya inayohojiwa kwa chini ya miezi sita kati ya miezi 12 iliyopita:
 - Watoto wachanga ambao wana umri wa chini ya miezi 6
 - Waliooana upya ambao wamekuwa wakiishi pamoja kwa chini ya miezi 6
 - Wanafunzi na wafanyakazi wa msimu ambao hawajakuwa wakiishi katika kaya nyingine, au kama sehemu ya kaya nyingine
 - Watu wengine wanaoishi [na kula] pamoja kwa chini ya miezi sita lakini ambao wanatarajiwa kuishi katika kaya [kwa jumla ya kipindi cha angalau miezi sita]
- Wahudumu, wafanyakazi shambani, na watu wengine kama hao wanaoishi na kula na kaya inayohojiwa wanapaswa kutambuliwa kama jamaa wa kaya hata ingawa hawana uhusiano wa damu [au wa kindoa] na kiongozi wa kaya

“Watu ambao wameishi katika kaya inayohojiwa kwa zaidi ya miezi sita kati ya miezi 12 iliyopita lakini ambao wameondoka kwenye kaya inayohojiwa (kwa mfano, kwa ajili ya talaka au kifo) *hawawezi* kuzingatiwa kama jamaa wa kaya inayohojiwa.

“Watu wanaoishi katika makazi sawia lakini hawashiriki gharama za chakula au wanakula milo pamoja *si* jamaa wa kaya inayohojiwa. Kwa mfano, ikiwa mwanamume ana wake wawili ambao (pamoja na watoto wao) wanaishi na kula pamoja, basi wote kwa pamoja wanatengeneza kaya moja, pia, ikiwa kila mmoja ya wake wa mwanamume huyo pamoja na watoto wao wanaishi na kula kivya, basi [kila kundi ni kaya tofauti]. Kwa njia sawia, ikiwa kaka wawili na kila mmoja ana familia yake binafsi na wanaishi pamoja katika nyumba sawia lakini hata hivyo wana bajeti tofauti, basi wanachukuliwa kama kaya mbili tofauti.

“*Jamaa wa kaya* wanabainishwa kama wale watu ambaao wamekuwa wakiishi katika kaya inayohojiwa kwa miezi sita au zaidi kati ya miezi 12 iliyopita. hata hivyo, watu waliokuja kuishi katika kaya kwa muda mrefu wanahesabiwa kama jamaa, hata kama wameishi katika kaya kwa chini ya miezi sita. Aidha, watoto waliozaliwa na jamaa wa kaya wakati wowote katika miezi 12 iliyopita wanahesabiwa kama jamaa wa kaya.

“Wale watu ambaao wangekuwa jamaa wa kaya lakini hawajakuwepo kwa zaidi ya miezi sita kati ya miezi 12 kwa ajili ya shule, kutafuta ajira, biashara, na mengine na ambaao wanaishi katika shule za mabweni, nyumba za kukodi, mabweni na mengine nchini Uganda wanapaswa kuhesabiwa kama jamaa wa kaya. Watu kama hao wanaoishi katika nchi za kigeni hawahesabiwi kama jamaa wa kaya inayohojiwa.

“Rekodi jamaa wa kaya kwa mpangilio ufuatao:

1. Mtu wa kwanza ni lazima awe kiongozi wa kaya, hata kama yeye siye mhojiwa na hata kama hayupo kwa muda tu
2. Jamaa wa familia ya karibu zaidi ya kiongozi (wake/waume na watoto) ambaao wanalala katika makazi na wanaokula milo pamoja. Ikiwa kuna zaidi ua mke mmoja, basi anza na mke wa kwanza, ikifuatiwa na watoto wake kulingana na umri, kisha mke wa pili na watoto wake kulingana na umri, na kuendelea hivyo
3. Watu wengine wanaohusiana na kiongozi wa kaya na mume/mke wake ambaao wanalala katika makazi na wanaokula milo pamoja
4. Watu ambaao hawayupo lakini kwa kawaida wanaishi na kula pamoja na kaya, yaani, wale ambaao hawajakuwepo kwa muda tu kwa zaidi ya miezi sita kati ya miezi 12 iliyopita kwa sababu za shule, kutafuta ajira, biashara, na mengine na ambaao ambaao wanaishi katika shule za mabweni, nyumba za kukodi, mabweni na mengine nchini Uganda
5. Watu ambaao hawana uhusiano ambaao wanalala katika makazi na wanaokula milo pamoja na kaya”

Kulingana na ukurasa wa 8 wa *Mwongozo*, “*Kaya inajumuisha mtu au kundi la watu, ambao wana uhusiano au bila uhusiano, wanaoishi pamoja katika makazi sawia, ambao wanamtambua mtu mmoja mzima ambaye ni mwanamume au mwanamke kuwa kiongozi wa kaya, ambao wanashiriki mipango sawia ya kuishi, na ambao wanazingatiwa kuwa kitu kimoja.*

“Wakati mwingine, unaweza kupata kundi la watu wanaoishi pamoja katika nyumba sawia, lakini kila mtu ana mipango tofauti ya kula. Katika tukio kama hilo, kila mkazi anapaswa kuhesabiwa kama kaya tofauti ya mtu mmoja.”

Kulingana na ukurasa wa 211 wa UBOS (2018), wewe kama mhoji unapaswa “kuomba orodha kamili ya jamaa wa kaya.” Wakati umetengeneza orodha ya kwanza, unapaswa kumwambia mhojiwa: “Ili tu kuhakikisha nina orodha kamili:

- Kuna watu wengine wowote kama vile watoto wadogo au watoto wachanga ambao hatujawaorodhesha?
- Kuna watu wengine wowote ambao huend wakawa si jamaa wa familia yako (kama vile wajakazi, wakodishaji, au marafiki) ambao kwa kawaida wanaishi [na kula] hapa?”

3. Kiongozi mwanamke (au mke mkubwa zaidi wa kiongozi mwanamume) anaweza kusoma na kuandika kwa ufasaha kwa lugha yoyote?

- A. Hakuna kiongozi mwanamke (wala mke wa kiongozi mwanamume)
- B. La
- C. Ndiyo

Swali hili linauliza kama kiongozi mwanamke (au mke mkubwa zaidi wa kiongozi mwanamume) anaweza kusoma *na* kuandika kwa lugha yoyote (kwa mfano, Kiingereza, Kiluganda, Kiswahili, Kirunyoro, Kirunyankole, Kirukiga, Kiluo, Kilusoga, na kadhalika).

Kumbuka kwamba tayari unajua jina la kiongozi mwanamke (au mke mkubwa zaidi wa kiongozi mwanamume) kutokana na kujaza “Karatasi ya Kazi ya Ukurasa wa Nyuma”. Hivyo basi, usiulize, “Kiongozi mwanamke (au mke mkubwa zaidi wa kiongozi mwanamume) anaweza kusoma na kuandika kwa ufasaha kwa lugha yoyote?”. Badala yake, tumia jina halisi la kwanza au jina la utani la kiongozi mwanamke (au mke mkubwa zaidi wa kiongozi mwanamume), kwa mfano: “Harriet anaweza kusoma na kuandika kwa ufasaha kwa lugha yoye?”

Ikiwa hakuna kiongozi mwanamke (au mke mkubwa zaidi wa kiongozi mwanamume) katika kaya inayohojiwa, basi usisome swalii hilo kamwe. Badala yake, weka alama kwenye jibu “A. Hakuna kiongozi mwanamke (wala mke wa kiongozi mwanamume” na uendelee na swalii linalofuatia.

Kwa madhumuni ya kadi hii ya alama, *kiongozi mwanamke (au mke mkubwa zaidi wa kiongozi mwanamume)* anabainishwa kama:

- Kiongozi wa kaya, ikiwa kiongozi ni mwanamke
- Mke/mwanandoa mkubwa zaidi wa kiongozi wa kaya, ikiwa kiongozi ni mwanamume
- Hayupo, ikiwa kiongozi ni mwanamume na ikiwa hana mke/mwanandoa ambaye ni jamaa wa kaya hii

Kulingana na ukurasa wa 12 wa *Mwongozo*, “*kiongozi wa kaya* ni mtu anayechukuliwa na jamaa wa kaya kama kiongozi wao. Mara nyingi, kiongozi wa kaya ni yule anayedhibiti mapato na gharama za kaya na ambaye ana maarifa zaidi kuhusu jamaa wengine wa kaya. Yeye atatajwa unapouliza swalii ‘Kiongozi wa kaya hii ni nani?’ Unapaswa kukubali uamuza wa jamaa wa kaya wanapomtambua kiongozi wao.

“Ni lazima kuwe na kiongozi mmoja pekee wa kaya. Endapo zaidi ya mtu katika kaya anadai kuwa kiongozi, au endapo jamaa wa kaya wanatoa kauli zinazokinzana kuhusu kiongozi wa kaya ni nani, basi kuna uwezekano mkubwa kwamba pale kuna kaya mbili au zaidi, badala ya moja. Katika tukio kama hilo, tumia vigezo vilivyotolewa vyatubaini ni nani jamaa wa kaya unayohoji.”

Kumbuka kwamba kiongozi wa kaya anaweza au akakosa kuwa jamaa wa kaya ambaye anashiriki katika mpango wako (ingawa kiongozi pia anaweza kuwa jamaa huyo).

4. Kuna jamaa yejote wa kaya anayeenda shule ya kibinaksi au shule ambayo inaendeshwa na shirika la kidini, NGO, au shirika lingine lolote lisilo la serikali?
- A. La
 - B. Ndiyo

Mwongozo huu haukupi maelezo ya ziada ya swali hili.

5. Katika miezi 12 iliyopita, kuna jamaa wa kaya aliyepata mapato kutokana na ukulima wa mimea au ufugaji mifugo?
- A. Ukulima wa mimea, lakini si ufugaji mifugo
 - B. Hakuna ukulima wa mimea wala ufugaji mifugo
 - C. Ufugaji Mifugo (bila kujali ukulima wa mimea)

Mwongozo huu haukupi maelezo ya ziada ya swali hili.

6. Aina ya nyenzo msingi iliyotumika sana katika ujenzi wa sakafu? (*kama ulivyoona*)
- A. Matope, matope maalum, mbao, au nyingine
 - B. Sementi na mchanga, zege, matofali, mawe ya matofali, au mawe

Kulingana na ukurasa wa 36 wa *Mwongozo*, wewe kama mhoji unapaswa ujaribu kutazama na urekodi nyenzo kuu ya ujenzi wa sakafu bila kumuuliza mhojiwa swali hili moja kwa moja. Ikiwa hauna uhakika kabisa kuhusu jibu, basi muulize mhojiwa swali hili.

Kulingana na ukurasa wa 37 wa *Mwongozo*, swali hili linarejelea sakafu ya nyumba kuu ya makazi. “Ikiwa zaidi ya nyenzo moja imetumika, rekodi aina ya nyenzo kuu (yaani, nyenzo iliyofunika sehemu kubwa zaidi ya sakafu). Ubora wa nyenzo yenyewe si muhimu. . . [Kumbuka ufafanuzi ufuatao]:

- *Sementi na mchanga*: Sakafu nyembamba iliyotengenezwa kwa kutumia mchanga na sementi
- *Zege*: Sakafu pana iliyotengenezwa kwa kutumia mawe yaliyovunjwa vunjwa na kuchanganywa na changarawe na sementi
- *Matope maalum*: Udongo uliochanganywa na maji, kupangwa na kuachwa ukauke”

Kulingana na ukurasa wa 36, “*Nyumba ya makazi ni nyumba ambayo inatumika na kaya.*”

7. Kaya inatumia aina ipi ya choo sana sana?

- A. Hakuna choo/kichaka/mifuko ya plastiki/ndoo/n.k., choo cha shimo (bila kifuniko na bila silabu), au nyininge
- B. Choo cha shimo (chenye kifuniko na/au silabu), Ecosan (choo cha mbolea), choo cha VIP, au choo cha maji

Kulingana na ukurasa wa 39–40 wa *Mwongozo*, “Swali hili linaluzia maelezo kuhusu aina ya choo kinachotumika na kaya. Linarejelea *matumizi* badala ya *umiliki*. . . . ikiwa kaya inatumia vyoo tofauti wakati wa mchana na wakati wa usiku, basi zingatia choo kinachotumika wakati wa mchana.

“Ufafanuzi wa vyoo:

- *Hakuna choo*: Wanatumia kichaka, au mifuko ya plastiki au ndoo
- *Choo cha shimo*: Uchafu unatupwa ndani ya shimo moja kwa moja bila kumwaga maji
- *Choo cha shimo kilicho na silabu*: Choo cha shimo kilicho na silabu, jukwaa au kiketi. Choo kina silabu iwapo sakafu ya choo hicho imetengenezwa na nyenzo gumu au laini ambao inaweza kusafika vizuri kabisa. Mifano ya nyenzo ya silabu ni sementi, mbao laini kabisa bila mianya, au mawe laini. Vyoo vilivyo na sakafu ya udongo, sakafu zilizofunikwa kwa matope, au sakafu za matope na vijiti havihesabiwi kama silabu. Si lazima silabu iwe imeinuliwa juu ya sakafu. Jukwaa au kiketi chochote ni lazima kime kimejishikilia imara kwa pande zote na kuinuliwa juu ya ardhi inayozingira ili kuzuia maji kuingia kwenye shimo na kwa ajili ya kusafisha kwa urahisi
- *Choo cha shimo bila silabu/cha shimo wazi*: Choo cha shimo bila silabu, jukwaa au kiketi. Shimo wazi ni shimo la kawaida ardhini ambapo uchafu unakusanyika
- *Choo cha shimo lililofunikwa*: Choo cha shimo chenye jengo la angalau kuta tatu na paa juu yake. jengo na paa hii zinazuia maji ya mvua kuingia chooni
- *Choo cha shimo bila kufunikwa*: Choo cha shimo ambacho hakina jengo juu yake. Choo cha shimo chenye jengo ambalo halina paa au bila kuta kinazingatiwa kuwa bila kufunikwa
- *Choo cha Ecosan*: Choo ambacho mavi na mkojo zinafanywa kuwa mbolea au kukaushwa (kwa kutumia jivu au nyenzo nyininge) kabla ya kutumika kwenye mazingira

- *Choo cha shimo kilichoimariswa kwa njia za hewa (VIP)*: Choo cha shimo ambacho kina bomba la hewa linalochomoza juu ya paa ya choo. Upande wa bomba ambao uko wazi umefunikwa kwa kichungi cha nyaya au neti isiyoruhusu nzi kupita, na upande wa ndani wa njengo hili unawekwa ukiwa na giza
- *Choo cha maji otomatiki/kumwaga maji*: Choo cha maji otomatiki kinatumia tangi la maji ya kusukuma uchafu na kina kizuizi cha maji (bomba lenye umbo la U) chini ya kiketi ambacho kinazuia nzi na uvundo kupita. Choo cha kumwaga maji pia kinatumia kizuizi cha maji lakini, tofauti na choo cha maji otomatiki, kinatumia maji ya kumwagwa kwa mkono ili kusukuma uchafu (tangi la maji halitumiki)”

8. Kwa sasa jamaa wa kaya wana simu ngapi za mkononi ambazo zinafanya kazi?

- A. Hakuna
- B. Mmoja
- C. Wawili au zaidi

Kulingana na ukurasa wa 42 wa *Mwongozo*, “*Umiliki* hapa unarejelea mali ya kibinafsi, bila kujali dhumuni ambalo simu ya mkononi inatumika. Simu yoyote ya mkononi iliyonunuliwa kwa deni itachukuliwa kuwa inamilikiwa.”

Kulingana na Hojaji ya UNHS ya mwaka 2016/17, ni simu za mkononi zinazofanya kazi pekee zinapaswa kuhesabiwa katika swali hili.

9. Kila jamaa wa kaya ana angalau kiatu kimoja ambacho ni kizuri kuvaliwa?

- A. La
- B. Ndiyo

Kulingana na ukurasa wa 45 wa *Mwongozo*, swali hili linalenga “kujua kama kila jamaa wa kaya ana viatu vilivyo katika hali nzuri. Sapatu, viatu vyatengenezwa na ‘tairi’ (*lugabire*), na gumboot hazizingatiwi kama viatu kwa madhumuni ya swali hili.”

10. Katika siku saba zilizopita jamaa wa kaya walipata wastani wa milo mingapi kwa siku?

- A. Mbili au chache
- B. Tatu au zaidi

Kulingana na ukurasa wa 45 wa Mwongozo, “Mlo ni kiwango kikubwa cha chakula, kinacholiwa kwa wakati mmoja. Inaweza kuwa katika tukio lolote la kawaida, kwa mfano, kiamsha kinywa, chakula cha mchana, au chakula cha jioni.”